Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 18, APRILI 2024







# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Emmanuel Malegi

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge
Aisha Swahibu
Atley Kuni

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

Dharura zaidi 60,000 zasafirishwa kupitia mfumo wa M-Mama ....UK 2





Barabara ya daraja la tanzanite kufungwa kila jumamosi asubuhi kupisha mazoezi .... UK 3

Huduma za utengamao kwa watoto wenye Usonji kuboreshwa - Waziri Ummy..... UK 4





Serikali kuanzisha taasisi mpya itakayo toa huduma za upasuaji wa Ubongo na Mishipa.... UK 5

Waziri Ummy alitaka baraza la wafanyakazi Wizara ya Afya kuimarisha ubora wa huduma .... UK 6





Kliniki maalum za magonjwa yasiyoambukiza zianzishwe kwenye vituo vyote vya afya nchini.... UK 6

Mifumo ya sekta ya afya kuimarishwa zaidi...... UK 7



Agenda ya kutokomeza malaria iwe ya kudumu katika vikao vya maamuzi .... UK 8





Serikali kuja na mtaala wa Lishe na afya ya Uzazi kwa vijana mashuleni na vyuoni. .... UK 9

Dkt. Jingu awataka madaktari bingwa kukaa vituoni.... UK 10





Watumishi 108 sekta ya afya wapigwa msasa kukabiliana na dharura za uzazi.... UK 11

Prof. Nagu ataka maoni yatakayo isadia sekta ya afya jumuiya afrika mashariki...... UK 12





Mabinti zaidi ya milioni tano kupa-tiwa chanjo ya Saratani ya Mlango wa Kizazi 2024 .... UK 13

Wananchi waipongeza serikali kuboresha miundombinu ya afya na huduma bora.... 14





Bilioni 3.8 kuimarisha utoaji wa huduma hospi-tali ya mkoa geita .... UK 15



Shahada ya sayansi ya mazoezi tiba kuboresha huduma za utengamao . .... UK 16

Madaktari sekoutoure wafaniki-sha kutoa jiwe la gram 800 kwenye kibofu cha mkojo.... UK 17





Wananchi jiridhisheni na uhalali wa vituo vya huduma za macho na miwani tiba..... UK 18

Zaidi ya wasichana milioni nne wenye miaka 9-14 kufikiwa na chanjo ya hpv..... UK 19





Hospitali mount meru yatakiwa kuimarisha ulezi vituo vya afya .... UK 20

Tuepuke tabia bwete kuk-abiliana na magonjwa yasiyoambukiza. ..... UK 21





Dozi moja ya chanjo ya hpv inatosha kumkinga msichana kupata saratani ya mlango wa kizazi.... UK 22



# Rais Samia kinara wa ajenda za kuinua Wanawake - Dkt. Mpango

**Na. Emmanuel Malegi**
**DAR ES SALAAM**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango amesema, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele kusukuma ajenda za kumkomboa mtoto wa kike kwenye changamoto zinazo mkabili.

Dkt. Mpango, ameyasema hayo alipokuwa akifungua mkutano wa masuala ya uongozi kwa wanawake kisekta Aprili, 06, 2024 jjiini Dar es salaam kwenye ukumbi wa kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere.

Amesema, uwekezaji mkubwa umefanywa kwenye Sekta ya Afya, Maji, Elimu na Nishati zimekuwa jitihada za makusudi za kumuinua mtoto wa kike kutokana na baadhi ya changamoto zilizokuwa zinawakabili kwa kipindi kirefu ikiwepo mila potofu pamoja na mfumo dume uliokuwa umeshamiri miongoni mwa baadhi ya jamii.

"Jitihada hizo upande wa Sekta ya Afya, kupitia huduma inayotekelezwa na mpango wa M-mama umewezesha kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa sasa." Amesema Dkt. Mpango

Kuhusu sekta ya maji, "Mhe. Rais amefanya jitihada za kumtua mama ndoo kichwani kwa kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwa uhakika na kumpunguzia adha mama kufuata maji umbali mrefu, kwani ameongeza bajeti ya maji kutoka shilingi bilioni 709.4 kwa mwaka wafedha 2022/23 hadi kufikia shilingi bilioni 756.2 kwa mwaka fedha 2023/24". Amesema Dkt. Mpango.

Dkt. Mpango amesema, Serikali imedhamiria kuwa na nishati safi na salama kwa mazingira salama kwa jamii, ambapo shabaha ya serikali nikuhakikisha ifikapo 2030 matumizi ya nishati iliyo safi na salama kwa mazingira inafikia asilimia 80 na hususan ni maeneo ya vijijini ambapo matumizi ya nishati isiyo rafiki imekithiri.

Kuhusu elimu Makamu wa Rais Dkt. Mpango, amesema zimekuwepo jitihada zenye tija kwa watoto wa kike kwa kuwajengea Shule Maalumu za Bweni ili waweze kuhitimu masomo yao na kufikia matamanio yao ya kile wanachotaka kufanya katika maisha yao.

"Wapo baadhi ya watoto wa kike walikuwa wamepata ujauzito na kujifungua watoto, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imehakikisha, wanarudi shuleni hata baada yakujifungua na kuendelea na masomo" Amesema Dkt. Mpango,

# Barabara ya daraja la Tanzanite kufungwa kila jumamosi asubuhi kupisha mazoezi

**Na. Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Barabara inayoanzia Taasisi ya Saratani Ocean Road kupitia Hospitali ya Aga Khan hadi kwenye daraja la Tanzanite itafungwa kila siku ya Jumamosi kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi kwa ajili ya kupisha mazoezi yatakayo saidia kupunguza magonjwa Yasiyoambukiza.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ametoa maelekezo hayo Aprili 28, 2024 baada ya kumaliza mbio za KM 5 za 'Run4Autism' (watoto wenye Usonji) zilizoanzia katika viwanja vya farasi kupitia daraja la Tanzanite Jijini Dar Es Salaam yenye lengo la kuchangia watoto wenye Usonji nchini Tanzania.

"Suala hili sio geni, ni sisi Tanzania ndio tulikua hatujaanza, tumeona nchi nyingi kubwa zinafunga barabara kwa muda ili kuruhusu watu kufanya mazoezi ya kukimbia na kutembea kwa uhuru mkubwa." Amesema Waziri Mkuu Majaliwa


Amesema, vyombo vitakavyoruhusiwa muda huo ni magari ya wagonjwa wa dharula (Ambulance) ambayo yataratibiwa na Mkuu wa Wilaya, baiskeli za mazoezi pamoja na pikipiki itakayotumika kumbeba mpiga picha kwa kibali maalum, wengine watapita barabara nyingine kwa muda huo.

"Mimi nimeshiriki marathon mara nyingi hapa Dar Es Salaam, nimeona wananchi wanavyojitokeza kwa wingi kufanya mazoezi ya viungo na kukimbia, wazee kwa vijana baada ya kupata elimu iliyosababisha kuhamasika kufanya mazoezi hivyo lazima kuwawekea mazingira rafiki ili wafanya mazoezi kwa uhuru." Amesema Majaliwa

Awali Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu aliiomba Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu kufungwa kwa barabara hiyo ili kuwapa uhuru watu wanaofanya mazoezi ya viungo, kukimbia na kutembea wafanye kwa uhuru.

"Mhe. Waziri Mkuu kama itakupendeza tunaomba barabara hii ya Tanzanite kila Jumamosi ifungwe kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi ili wa muda huo iweze kutumika kwa ajili ya mazoezi." Ametoa ombi hilo Waziri Ummy.





# Ajenda ya kutokomeza malaria, Rais Samia ameonesha imani - Dkt. Kikwete

**Na Atley Kuni,**
**ARUSHA**

Rais Mstaafu wa Awamu ya nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amesema Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonesha imani kwa viongozi aliowateua kusimamia baraza la kuongoza mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria hivyo hawana budi kuja na afua zitakazo iwezesha nchi kufikia azma yake ya kutokomeza Malaria.

Dkt. Kikwete ambaye ni Mjumbe wa kamati ya Dunia wa amesema hayo Aprili 13, 2024 jijini Arusha wakati wa ziara yake kwenye kiwanda cha kuzalisha vyandarua kilichopo mkoani humo cha A to Z.

“Miongoni mwa wajumbe tulioteuliwa na Rais ni watu ambao tumeshafanya mambo makubwa katika jamii, hivyo imani ya Mhe. Rais ni kubwa kwetu tunasema, alitupa imani, hivyo ni vyema tukamlipa imani, ni rai yangu tuoneshe fadhila kwa kushirikiana na jamii kuja na afua zitakazo wezesha kufikia azma". Amesema Dkt. Kikwete.

Aidha, Dkt. Kikwete amesema kuanzia sasa nchi ni lazima ianze kuwaza kwenye kuzuia na kutokomeza kabisa Malaria ikiwemo kutekeleza afua kama vile kuua viluilui vya mazalia ya mbu ambayo ni chanzo kikuu cha ugonjwa huo

Ameongeza kuwa, Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 zilizo kwenye maambukizi makubwa ya Malaria, huku bara la Afrika likiwa linaathiriwa na malaria kwa asilimia 93 na asilimia saba ndio nchi zingine za dunia.

“Takwimu hizi sio nzuri kabisa, hivyo lazima tuje na majibu ya kisayansi kwa masuala haya ya kisayansi, katu tusilete siasa, wenzetu A to Z hapa Arusha wameonesha mfano na nilipokuwa na wajumbe wenzangu wa Dunia wakanituma nije nitembelee kiwanda hiki na kwakweli nimejionea kazi wanayofanya ni njema". Amesema Dkt. Kikwete.

Akitoa salaam za Wizara Dkt. Catherine Joachim amesema zipo sababu kadhaa zinazo changia kufanya usugu kwenye mwili wa mtu hasa matumizi yasiyo sahihi ya dawa.

“Kuna baadhi ya watu akiugua bila hata kupima anakwenda kununua dawa na kumeza lakini wakati mwingine watu kutokumaliza dozi wanazo andikiwa na wataalam, hii imekuwa ni changamoto hivyo tunawashauri watu pindi asikiapo dalili za ugonjwa ni vema akawaona wataalam akapima ndio ameze dawa” amesema Dkt. Catherine.
Pia amemshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya kutokomeza Malaria nchini kwa jitihada anazo chukua kama mtanzania kuhakikisha mipango ya Serikali kutokomeza Malaria ifikapo 2030 inatimia.

# Bohari ya Dawa yaungwa mkono na kamati ya Bunge ya Bajeti

**Na Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti Mhe. Oran Njeza ameahidi kupitia Kamati yake kuiunga mkono Wizara ya Afya kupitia Bohari ya Dawa (MSD) kwa kujenga maghala na viwanda vya dawa ili kupunguza gharama za kuagiza dawa hizo kutoka nje ya nchi.
Mhe. Njeza amesema hayo jioni ya Aprili 30, 2024 wakati wa kikao cha kamati ya Bunge ya Bajeti baada ya wasilisho la mpango kazi wa Bohari ya Dawa (MSD) kuhusu ujenzi wa viwanda vya dawa na maghala ya kuhifadhia dawa.

"Tunaipongeza sana Wizara ya Afya, tunaiunga mkono MSD kwa kuwa ni azimio la Bunge ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hizo za dawa kwa wananchi." Amesema Mhe. Njeza
Aidha, Wabunge hao wamempongeza Waziri Ummy kwa kuwa anasema na anatenda kwa yale anayoyaahidi pamoja na kuishauri MSD kufanya utafiti wa dawa chache ambazo ni muhimu na zitajitaji ndio ziagizwe nje ili kupunguza uwgizwaji wa dawa hizo nje ya nchi na kuweka nguvu katika kutumia Tiba Lishe.

Kwa upande wake Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inatoa asilimia 50 ya fedha za Dawa kwa MSD ambapo kwa ime - pokea kiasi cha Bilioni 100 kwa ajili ya kulipa deni la MSD ambalo Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha zimekunaliana kubadilishwa na kuwa kama mtaji.

Waziri Ummy amesema, miongoni mwa hatua zitakazo chukuliwa kwa Bohari ya Dawa ni pamoja na kubadilisha muundo wa MSD ambapo Mkurugenzi Mkuu atashuhulika na masuala ya kununua na kutunza bidhaa za dawa na mengine watawaachia Sekta binafsi pamoja na kuzipa kipaumbele dawa za asili kwa maana magonjwa mengine unapona bila kutumia dawa za 'antibiotics'.

Nae, Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD) Bw. Mavere Tukai wakati akiwasilisha mpango kazi huo amesema hadi kufikia Machi 30, 2024, MSD ilikuwa na mita za mraba 36,254 na mahitaji ya ziada yakiwa ni mita za mraba 63,746.

"Katika kuhakikisha Bohari ya Dawa inafanikisha majukumu yake ya msingi, tunapendekeza Bohari ya Dawa isaidiwe kwa kupewa vyanzo vitakavyowezesha kupata mkopo wenye masharti nafuu (concessional loan) utakaosaidia ujenzi wa maghala." Amesema Bw. Mavere



# Tuchukue hatua, tuwekeza kwenye afya zetu - Waziri Ummy




**Na. Eglibert Kayombo**
**DAR ES SALAAM**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amewataka Watanzania kuchukua hatua kwa kuwekeza kwenye Afya zao na kufuata ushauri wa wataalamu wa Afya ikiwemo kufanya mazoezi ili kuepukana na Magonjwa yasiyoyakumbukiza.

Waziri Ummy amesema hayo Aprili 13, 2024 baada ya matembezi ya hisani ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya siku ya Afya Dunia yaliyoanzia katika ofisi za Shirika la Afya Dunia (WHO) hadi daraja la Tanzanite Jijini Dar Es Salaam.

"Tumeona wagonjwa wengi wenye Shinikizo la Juu la Damu na Kisukari, kama kweli tunataka Afya zetu ziwe salama lazima kila mmoja aanze kuchukua hatua ili tuepuke magonjwa Yasiyoambukiza". Amesema Waziri Ummy
Amesema, Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kuchukua hatua za makusudi za kuwekeza kwenye miundombinu ya kutoa huduma za Afya ikiwemo kujenga Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za ngazi zote pamoja na kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi ikiwemo huduma za maabara. Amesema Waziri Ummy

"Serikali inaendelea kuwekeza katika upatikanaji wa rasilimali watu wa Afya kwa ngazi zote kuanzia huduma za Afya za msingi hadi huduma za ubingwa na ubingwa bobezi, kuimarisha upatikanaji wa dawa pamoja na kuwekeza kwenye elimu ya Afya kwa Umma". Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy amesema katika kila Watanzania 100, Nane tu ndio wana bima za Afya hali ambayo inasababusha kuelemewa kwa mifuko hiyo kwa kuwa ndio inaendesha Sekta ya Afya ikiwemo Hospitali za Serikali na Hospitali binafsi.

"Ili kufikia lengo la Afya kwa wote, Serikali inajikita katika kuhakikisha tunaimarisha mifuko ya bima ya Afya ikiwemo mfuko wa NHIF pamoja na mifuko ya Bima binafsi ili Watanzania wengi waweze kuwa na bima za Afya." Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy ametoa wito kwa makampuni ya Bima za Afya kuanzisha mipango ya kuwa na bima ya Afya kwa Watanzania ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi hasa wananchi wa kipato cha chini pindi wanapougua.



# Huduma za utengamao kwa watoto wenye Usonji kuboreshwa - Waziri Ummy

**Na. Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Na. WAF - Dodoma
Serikali kupitia Wizara ya Afya imeanza kuchukua hatua madhubuti ili kuongeza nguvu katika uboreshaji na upatikanaji wa huduma za Utengamao kwa watoto wenye Usonji pamoja na watoto wenye ulemavu ikiwemo kuongeza idadi ya wataalamu wa huduma za Saikolojia Tiba (Clinical Psychology).

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo Aprili 3, 2024 kwenye kurasa zake za mitandao ya kijamii (X, Instagram) baada ya kumsikiliza Mzazi wa mtoto mwenye Usonji Bi. Hamida Michael aliyerekodiwa na Azam Tv.

“Nimeguswa na taarifa hii ya Mama Hudhaifa na hali hi inawakabili wazazi wengi nchini kwetu hususani wanawake wanaolea watoto wenye Ulemavu ikiwemo Watoto wenye Usonji.” Amesema Waziri Ummy

Amesema, ni kweli bado Tanzania haijafanya vizuri sana katika upatikanaji wa huduma za utengamao hususani kwa watoto ikiwemo watoto wenye Usonji pamoja na watoto wenye ulemavu kwa ujumla, lakini Serikali inaendelea na juhudi mbalimbali ili kuboresha huduma hizo.

“Tumeanza kuchukua hatua mahususi ili kuongeza nguvu za kuboresha na kusogeza upatikanaji wa huduma za Utengamao kwa watoto wenye usonji na watoto wenye ulemavu kwa ujumla ikiwemo kuongeza idadi ya wataalamu wa huduma za Utengamao hususani Huduma za Saikolojia Tiba (Clinical Psychology).” Amesema Waziri Ummy

Amesema, hatua nyingine zinazochukuliwa ni pamoja na mazoezi tiba (Physiotherapy), mazoezi kazi (Occupational Therapy), huduma za mawasiliano na kuongea (Speech and Communication Therapy) sambamba na kuweka miundombinu na Vifaa Tiba kwa ajili ya huduma za Utengamao kwa watoto, wazee na watoto waliopata Kiharusi. Waziri Ummy ametoa pongezi kwa Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili kwa kuanzisha kozi mbalimbali za ngazi ya Shahada ya kwanza (Degree) katika Huduma za Utengamao na Afya ya Akili ambayo itasaidia kupunguza tatizo la Usonji nchini.

“Naamini hatua tulizoanza kuzichukua zitatuwezesha kuwafikia watoto wengi ili waishi maisha bora zaidi na kuweza kujitegemea na kushiriki katika shughuli za uzalishaji Mali.” Amesema Waziri Ummy

# Serikali kuanzisha taasisi mpya itakayo toa huduma za Upasuaji wa Ubongo na Mishipa

**Na Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imedhamiria kuanzisha Taasisi mahususi ambayo itakuwa inashuhulikia masuala ya upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu ili iweze kuboresha zaidi huduma hizo za ubingwa kuitoa katika Taasisi ya Mifupa Ubongo (MOI) ambapo itabakia na masuala ya upasuaji wa mifupa pekee.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo Aprili 27, 2024 baada ya uzinduzi wa chama cha madaktari bingwa wa ubongo na mishipa ya fahamu (Tanzania Neurosurgical Society) kikiongozwa na Rais wa chama hicho Dkt. Othmani Kiloloma Jijini Dar Es Salaam.

"lengo la chama hichi ni kuunga mkono jitihada za Serikali za kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora na salama za upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu, ikiwemo upatikanaji wa madaktari bingwa wa upasuaji ubongo na mishipa ya fahamu". Amesema Waziri Ummy

Amesema, Tanzania kuna madaktari bingwa wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu 25 tu, ambapo kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) inapendekeza angalau katika kila watu 150,000 kuwe na daktari bigwa wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu Mmoja.

"Ukichukua idadi ya madaktari bigwa wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu 25 tulionao maana yake kwa Tanzania daktari bigwa Mmoja anahudumia Watanzania Mil 2,400,000, huduma hizi bado hazijawafikia Waanzania wengi ndio maana chama hichi kimekuja ili pia kujengeana uwezo na kuhamasisha madaktari wengine waweze kusomea fani hiyo ya upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu". Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy amesema, Serikali inaendelea kuboresha huduma za Afya ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za kibingwa, usambazaji wa maafisa wa Afya katika vituo vyote vya Afya na Hospitali, uanzishwaji wa huduma za kina za upasuaji katika Hospitali za Rufaa za Kanda na ukuzaji wa wataalamu wadogo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa.

"Lakini pia Serikali imeendelea kuweka msisitizo wa elimu endelevu katika taaluma za upasuaji ikiwa ni pamoja na upasuaji wa Neurosurgery, Neuro-radiology, Neuropathology, Neuro-anesthesiology, critical care, Neurology, pamoja na Neuro-rehabilitation". Amesema Waziri Ummy

Pia, Waziri Ummy amesema Serikali imeendelea kuimarishwa upatikanaji mkubwa wa huduma za uchunguzi kupitia CT-scan katika Hospitali zote za Rufaa za Kanda pamoja na ujumuishaji wa huduma za MRI na huduma za 'Angiography' katika vituo vya ngazi ya juu ili kumrahishia Mtanzania kupata huduma hizo za uchunguzi ndani ya nchi.





# Waziri Ummy alitaka baraza la wafanyakazi Wizara ya Afya kuimarisha ubora wa huduma

**Na Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, ameliambia Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Afya kugeukia na kuboresha kipengele cha ubora wa huduma kwa wananchi ili azma ya Serikali ya kufikisha huduma bora kwa wananchi mahala walipo iweze kufanikiwa.

Waziri Ummy ametoa wito huo Aprili 04, 2024 wakati wa kikao cha baraza hilo lililokutana kwa siku moja jijini Dodoma kwa ajili ya kupitia ya utekelezaji na ufafanuzi wa hoja mbalimbali pamoja na mikakati ya kutoa huduma bora kwa wananchi sambamba na kujadili bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24 na 2024/25.

Waziri Ummy amelitaka baraza hilo, kuhakikisha linakuwa chombo sahihi cha kumshauri yeye na menejimenti ya Wizara ili changamoto zinazoikabili sekta ya afya ziweze kusuluhishwa kwa pamoja.

"Tunajua tumefanya vizuri sana kwenye miundombinu na vifaa tiba, lakini tumeendelea kulalamikiwa kwenye eneo la huduma na hususan ngazi ya msingi, huku juu kwenye kanda na ngazi ya hospitali za Rufaa za mikoa, tumejitahidi sana. Rai yangu kwenu tuendelee kusaidia katika kuimarisha huduma kwenye Zahanati, Hospitali za Wilaya na Vituo vya afya". Amesema Waziri Ummy.

"Jambo tukishakubaliana kwenye vikao halali, tunatakiwa kwenda kwenye utekelezaji, tunapoendelea kuzunguka na kupiga dana dana tunawakwamisha wananchi na mwisho wa siku tunalaumiwa. Niliombe baraza hili, mnapojadiliana suala hili mlipe kipaumbele". Amesema Waziri Ummy.

Katika hatua nyingine Waziri Ummy ametumia Baraza hilo kuhimiza matumizi ya TEHAMA kwenye Sekta ya Afya, kwani ndio suluhu itakayo wezesha kuepusha udanganyifu, ikiwa pamoja na vipimo kurudiwa rudiwa, lakini pia matumizi mabaya ya vifaa tiba kama CT Scan.

Awali Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu wakati akimkaribisha Waziri Ummy amemueleza kuwa kikao hicho kitajadili mada mbalimbali zikiwemo uwasilishaji wa bajeti, taarifa ya utekelezaji wa hoja mbalimbali za watumishi, rasimu ya miundo ya utumishi wa kada ya afya, utendaji kazi katika utumishi wa umma, Mkakati wa utoaji wa huduma na utendaji kazi wa wizara katika kuboresha huduma za Afya.

# Agenda ya kutokomeza Malaria iwe ya kudumu katika vikao vya maamuzi




**Na Atley Kuni**
**TABORA**

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amezi-asa Kamati za Ulinzi na Usalama nchini kuona umuhimu wakuifanya ajenda yakutokomeza Malaria iwe yakudumu kwenye vikao vya maamuzi.

Dkt. Mollel ameyasema hayo , Aprili 25, 2024 akiwa amemwakilisha Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu kwenye kilele cha Siku ya Malaria Duniani iliyofanyika mkoani Tabora na kusema kuwa kama nchi imeendelea kupiga hatua katika vita hivyo ikilinganishwa na miaka zaidi ya ishini iliyopita ambapo maambuki na vifo vya Malaria vilikuwa kati ya asilimia 45 hadi 50.

Aidha Dkt. Mollel amesema azma ya Serikali ni kufikia asilimia 3.5 ifikapo 2025 na kuwa na ziro Malaria 2030 huku akisisitiza kwa kusema itafikiwa endapo juhudi za Makusudi zitafanywa kwa ushirikiano baina ya Serikali na wadau

" tunazungumza asilimia 8.1 kama nchi lakini miaka ya 1998, tulikuwa na kiwango cha juu sana, hivyo ili tuweze kufikia adhma yakumaliza kabisa malaria ifikapo 2030 kila mmoja wetu anawajibu wakufanya" amesema Mollel.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Afya Ofisi ya Rais TAMISEMI Samsoni Maella, amesema Utumiaji wa Mifumo ya GoTHOMIS na FFARS imekuwa chachu ya kukusanya takwimu sahihi kwa ajili ya ngazi ya maamuzi, hali iliyochangia kufanya maamuzi sahihi kutokana na kuwa na takwimu sahihi.

"Kama Ofisi ya Rais TAMISEMI, tumefanikiwa kuimarisha miundo mbinu ya Afya na Rasilimali watu mathalani miaka mitatu nyuma tulikuwa na Hospitali za Wilaya 77  hii tunazo 177 hizi zimechochea sana uimarishaji wa huduma" amesema Mahela.

Naye Mjumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Afya na Maswala ya UKIMWI Dkt. Hamis Kig-wangala ametoa wito kwa serikali na wadau kuongeza afua za kutibu watoto Shuleni, pia wafike maeneo ya Migodi, Mashamba Makub-wa na maeneo ya Wafugaji.

Awali Msimamizi wa Miradi kutoka Wizara ya Afya Dkt. Catherine Joachim, akiwa amemwak-ilisha Katibu Mkuu, amesema kuchaguliwa kwa mkoa wa Tabora kuwa mwenyeji wa Maadhi-misho ya Wiki ya Malaria, ni pamoja na kuonge-za nguvu ya afua za kupambana na Malaria kutokana na Mkoa huo kuwa na Maambukizi ya juu ya Ugonjwa huo ya asilimia 23.4 kwa sasa kutoka asilimia 11.7 kwa mwaka 2011.



# Tanzania yapokea shilingi bilioni 45 kuboresha Uzazi wa Mpango

**Na Majid Abdulkarim**
**DAR ES SALAAM**

Serikali ya Uingereza imeendelea kuimarisha ushirikiano wake na Tanzania kwa kutoa shilingi Bilioni 45 ili kusaidia kufanikisha huduma za uzazi wa mpango nchini.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel wakati wa hafla ya kumpokea Waziri wa Maende na Maswala ya Afrika kutoka Uingereza, Mhe. Andrew Mitchell, aliyetembelea Zahanati ya Vingunguti na kujionea huduma za uzazi wa mpango zinavyotolewa.

Dkt. Mollel ameeleza kuwa ufadhili huo ni matunda mazuri ya juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuimarisha ushirikiano na mataifa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Uingereza.

"Kupanga uzazi ni sehemu muhimu ya afya ya mama na mtoto, inayosaidia jamii kupata nafasi ya kuzingatia uzazi na kuhakikisha usalama wa mama na mtoto unapatikana kwa kuacha nafasi baina ya mtoto mmoja na mwingine, hasa katika kipindi cha unyonyeshaji, ili kila mtoto apate muda sahihi wa kunyonya pale anapozaliwa". Amesisitiza Dkt. Mollel.

Aidha, Ameishukuru Serikali ya Uingereza kwa ufadhili huo na kusema kuwa Tanzania itahakikisha jamii inapata elimu sahihi kuhusu uzazi wa mpango ili fedha hiyo itumike kusaidia wananchi katika kupanga uzazi.

Waziri wa Maende na Maswala ya Afrika kutoka Uingereza, Mhe. Andrew Mitchell, amesema kuwa lengo la ufadhili huo ni kuwawezesha Watanzania, hususan vijana kufanya maamuzi sahihi kuhusu wakati wanapotaka kuwa na watoto ili kuhakikisha shughuli za uzazi hazikwamishi shughuli za maende nchini.

"Kupitia ufadhili huu, vijana watapata elimu ya kujikinga na maradhi mbalimbali kama vile UKIMWI na kuelewa umuhimu wa kutumia uzazi wa mpango katika familia zao ili kusaidia taifa kuwa na mpangilio mzuri wa watoto kupishana na kupeana muda wa kunyonya. Ameeleza Mhe. Mitchell.

# Dkt. Jingu awataka madaktari bingwa kukaa vituoni

**Na Abdulwaheed Madenge**
**KILIMANJARO**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amewataka Madaktari Bingwa nchini kukaa katika vituo vyao vya kazi walivyopangiwa ili kuwezesha wananchi kupata huduma za kibingwa katika maeneo yao.

Dkt. Jingu amesema hayo wakati akizungumza na watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mawenzi iliyopo mkoani Kilimanjaro ikuwa ni sehemu ya ziara yake kuangalia hali ya utoaji wa huduma za afya.

Dkt. Jingu ameipongeza Hospitali hiyo kwa huduma bora inazotoa kwa wananchi huku akiwataka Madaktari bingwa kujitoa zaidi kuwasaidia wananchi na kuwataka wauguzi kuwatumia vyema madaktari hao katika kushauriana namna ya kuwahudumia wananchi ili kufikia azma ya utoaji bora wa huduma za afya.

“Ni vizuri wataalam wa afya mkashauriana namna masuala mbalimbali ya taaluma na kupeana uzoefu, Serikali imewekeza kwenye miundombinu, watumishi, vifaa na vifaa tiba lengo likiwa ni kutoa huduma za afya kwa wananchi wanaohitaji huduma hizo hivyo kupitia nyie wataalam huduma zitaendelea kuimarika”. Amesema Dkt. Jingu.

Aidha, Dkt. Jingu amesema kuwa wananchi hivi sasa wanahitaji huduma za kibingwa hapa nchini ili waweze kuokoa gharama za kufuata huduma hizo nje ya nchi, hivyo ili huduma hizo ziweze kupatikana kwa ufanisi zinahitaji uwepo wa wataalam wakiwemo Madaktari na bobezi.

Hata hivyo Dkt. Jingu amesema Hospitali ya Rufaa ya Mkoa mawenzi ina jukumu wa kuzilea Hospitali zilizo chini yake huku akionesha kufurahishwa na dawati la huduma kwa wateja na kusisitiza kuwa lugha nzuri ndiyo muhimili mkuu wa mawasiliano kwa wananchi huku akiongeza Serikali ina matumaini makubwa na watumishi na pia wajitahidi kuongeza ubunifu kwa kila wanachokifanya na kuangalia huduma za kuongeza ili Hospitali iwe bora zaidi.



# Watumishi 108 sekta ya Afya wapigwa msasa kukabiliana na Dharura za Uzazi



**Na Aisha Swahibu**
**MARA**

Watumishi 108 wa Afya kutoka kwenye vituo vya Afya vipatavyo 25 kati ya 37 vinavyotoa huduma ya upasuaji wa mtoto, mkoani Mara wamejengewa uwezo maalum kwa ajili yakukabiliana na dharura za uzazi pindi zitokeapo.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe amesema kuwa mafunzo watakayopewa watumishi hao ni msisitizo katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Dkt. Magembe ameyasema hayo Aprili 19, 2024 alipokuwa akifungua Mafunzo ya kukabiliana na dharura zitokanazo na uzazi Mkoa wa Mara.

"Haya mafunzo yanakuja kufanyika kwenu nyinyi watumishi wa afya ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na dharura za uzazi kwasababu kinacho tutofautisha sisi watumishi wa sekta ya afya na sekta nyingine ni suala la dharura kumsaidia mama kurudi katika hali yake pale anapopata changamoto ya uzazi" Amesema Dkt. Magembe

Dkt. Magembe amesema huo ni mwanzo lakini shabaha nikuhakikisha mafunzo hayo yanafanyika nchi nzima hasa kwenye vituo vinavyotoa huduma ya wajawazito kujifungua.

Katika hatua nyingine Magembe amesema mbali ya kuwapatia mafunzo pia itafanyika tathimini na ufuatiliaji wa mafunzo hayo kwa njia tehema ili kuwezesha kuboresha huduma za afya.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara Dkt. Zabron Msatu amesema kuwa kupitia mafunzo haya yatawezesha kupunguza vifo vya mama na mtoto na kufikia malengo ya kitaifa na kidunia ambayo yamewekwa kwa kuhakikisha wanaongeza ujuzi kwa watumishi ili kuongeza ujuzi katika vituo takribani 37 vya kutoa huduma za dharura ndani ya Mkoa wa Mara.

Kulingana na Takwimu za Januari hadi Disemba 2023, kati ya wajawazito 103,478 waliojifungua kwenye vituo 344 vya Mkoa wa Mara, 42,444 sawa na asilimia 41%, walijifungua kwenye vituo hivyo 25 vya CEmONC vilivyochaguliwa, ambapo ninyi washiriki wa mafunzo haya mnafanya kazi.



# Prof. Nagu ataka maoni yatakayo isadia sekta ya Afya Jumuiya Afrika Mashariki

**Na Atley Kuni**
**DAR ES SALAAM**

Mganga Mkuu wa Serikali wa Prof. Tumaini Nagu, ametoa rai kwa wataalamu wa sekta ya Afya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kutoa maoni yatakayosaidia Jumuiya kuimarisha miundombinu ya huduma ya afya na kukabiliana na matishio ya kiafya kwa magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

Prof. Nagu ametoa kauli hiyo Aprili 30,2024 Jijini Dar Es Salaam katika ufunguzi wa Mkutano wa Kawaida wa 24 wa Baraza la Mawaziri wa sekta ya Afya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) .

"Tumekuja kujadili na kutoa suluhisho na majawabu yatakayo wezesha kukabili changamoto za kiafya ndani ya nchi za Jumuiya yetu kwa kuzingatia ubunifu na weledi wa mifumo yetu ya afya huku tukiwa na umoja wenye nguvu zaidi" amesema Prof. Nagu

Prof. Nagu amehimiza umuhimu wa Sekta ya Afya kwa Jumuiya kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi na umoja wakati wa utekelezaji progamu mbalimbali za Afya ikiwemo miradi ya Sekta ya Afya na mikakati inayopangwa ili kufikia mafanikio yanayotarajiwa kwa wakati.

Mbali na kufanya tathimini ya utekelezaji wa maagizo na makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano wa 22 wa Baraza hilo, Mkutano huo utajadili agenda nyingine ikiwemo Mkutano na taarifa za Vikundi Kazi (Technical Working Group – TWG) sita (06) vya Sekta ya Afya na mapendekezo ya Tanzania kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Upandikizaji Uloto na Sayansi ya Matibabu ya Magonjwa ya Damu chini ya Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Sekta ya Jamii wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Dkt. Irene Isaka, ameeleza kuwa kupitia mkutano huo nchi wanachama watapata fursa ya kusikia taarifa zitakazowasilishwa na kila nchi ili kwa pamoja kuweza kuchangia na kushauri namna bora ya kusimamia na kutekeleza programu, miradi na miundombinu ya Afya katika Jumuiya.

Mkutano huo wa siku tano, unafanyika kwa njia ya mseto (video na ana kwa ana) umeanza kwenye ngazi ya wataalam ukilenga kufanya tathimini ya utekelezaji wa maagizo na makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano wa 22 wa Baraza hilo.



# Mabinti zaidi ya milioni tano kupatiwa chanjo ya Saratani ya Mlango wa Kizazi 2024

**Na Shaban Juma**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imepanga kuendelea utoaji wa chanjo kwa watoto zaidi ya milioni tano ya ugonjwa wa Saratani ya mlango wa kizazi (HPV) kwa mabinti wa miaka tisa hadi kumi na nne ili kuwakinga na vimelea vya ugojwa huo.
Hayo yamesemwa na Kaimu Mkurugenzi wa kitengo cha elimu ya Afya kwa umma Dkt. Tumaini Haonga tarehe 13 Aprili, 2024 wakati wa semina ya waandishi wa habari kuhusu chanjo ya Saratani ya mlango wa kizazi jijini Dodoma.

Amesema, chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi itatolewa kwa mabinti zaidi ya milioni tano wenye umri wa kuanzia miaka tisa hadi kumi na minne kwa dozi moja ambapo awali ilikuwa ikitolewa kwa watoto wenye umri wa miaka kumi na minne tu kwa dozi mbili.

"Kufuatia tafiti ya WHO na kwa kuzingatia mingozo ya wizara yetu ya afya imeona chanjo ya HPV inaweza kuwa na ufanisi wa kutosha kwa kumkinga mtoto kutokana na vimelea vya saratani ya mlango wa kizazi hata kwa dozi moja, ambapo awali tulikuwa tunawapatia dozi mara mbili, nitoe rai kwa watanzania kuwatoa watoto hao ili kuweza kupatiwa chanjo hii". Amesema Dkt. Haonga.

Aidha, Dkt. Haonga amevitaka vyombo vya habari kote nchini kutumia taaluma zao kuhamasisha na kuelimisha na kuwapa ufafanuzi wananchi juu ya masuala mazima ya afya hususani kuhusu ugonjwa wa saratani na mlango wa kizazi na chanjo yake kwa sababu wananchi wengi wanategemea kupata taarifa kupitia vyombvo vya habari.

"Nitoa wito kwa wanahabari kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuhakikisha taarifa, elimu na uhamasishwaji wa jamii kuhusu chanjo hii zinawafikia watanzania, ninyi wanahabari mna vyanzo vingi vinavyoweza kuwafikia watanzania kwa wingi hivyo mkatoe taarifa kuhusu afya ili kufikia dhima ya Serikali ya kuwakinga wananchi na saratani ya mlango wa kizazi na kuhakikisha tunakuwa na taifa lenye afya bora". Amesisitiza Dkt. Haonga.

Pia amewasisitiza watanzania wote kuwa na desturi ya kupima afya zao mara kwa mara ili kuwahi kuchukua hatua stahiki pindi wanapobainika wana changamoto ya ugonjwa.

# Wananchi waipongeza Serikali kuboresha miundombinu ya Afya na huduma bora

**Na Shaban Juma**
**LINDI**

Wananchi wameipongeza Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt Samia Suluhu kwa Maendeleo ya Miundombinu ya Afya na huduma bora katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Hayo yamejiri kufuatilia ziara ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe alipotembelea mikoa ya Mtwara na Lindi kwa ajili ya kukagua miradi ya ujenzi, vifaa, vifaa tiba, ubora wa huduma pamoja na kuongea na watumishi wa sekta ya afya.

Harouni Selemani Harouni akiwakilisha wananchi amesema huduma ambazo zinatolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya zimekuwa nzuri kuanzia mapokezi mpaka kupata huduma wananchi wameonyesha furaha na pongezi kwa serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan kufuatia jitihada zake za kuboresha miundombinu kuleta vifaa vya kisasa kwa ajili ya huduma za afya nchini.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Dkt Grace Magembe amewapongeza watumishi wa afya kwa kutoa huduma bora kwa wananchi na hili limeonekana kwa mwitikio wa wananchi kufuatia upatikanaji wa huduma hasa huduma kwa wateja.

"Wananchi wanapozungumza huwa wanazungumza ya moyoni kabisa, ikiwa mmefanya vibaya watasema mkimfanya vizuri watawapongeza vilevile na nimeona wengi wanawapongeza, sijaona wananchi wakiwasema vibaya sana sana wanazungumzia upungufu ya watumishi ". Amesema Dkt Magembe

Dkt. Grace Magembe amesisitiza umuhimu wa kutoa huduma bora kwa wananchi na kuendelea kutoa huduma bora kwa wateja na kuwahimiza watumishi hao kuzingatia maadili ya kazi na kujituma katika kutoa huduma kwa wananchi.

"Serikali inaendelea kutekeleza ahadi zake za kuboresha sekta ya afya na kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata huduma bora za afya hivyo sisi kama watumishi katika sekta ya afya ni jukumu letu kuwahudumia kwani maboresho aliyofanya Dkt. Samia Suluhu Hassan ni makubwa". Amesema Dkt Magembe



# Bilioni 3.8 kuimarisha utoaji wa huduma Hospitali ya mkoa Geita

**Na. Majid Abdulkarim**
**DODOMA**



Serikali imepeleka vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za Afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel  Aprili 29, 2024 Jijini Dodoma wakati akijibu swali Namba 198 kutoka kwa Mbunge wa Viti Maalum Mhe. Josephine Tabitha Chagula aliyeuliza Je, lini Serikali itapeleka Watumishi pamoja na Vifaa Tiba katika Hospitaliya Mkoa wa Geita.

Dkt. Mollel amesema Hospitali ya Mkoa Geita ina jumla ya watumishi 349 na katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepeleka watumishi 22 wa kada mbalimbali katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Geita ili kuendelea kuimarisha utaoji wa huduma za afya katika Hospitali hiyo.






# Shahada ya sayansi ya mazoezi tiba kuboresha huduma za Utengamao

**Na Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Na WAF - Dar Es Salaam
Serikali kupitia Wizara ya Afya ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Muhimbili (MUHAS) imeanzisha Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Mazoezi Tiba ili kusaidia mawasiliano (Speech pathology), Tiba Kazi (Occupational therapy) na Tiba Viungo (Physiotherapy) kuanzia mwaka 2024 ili kuboresha huduma za utengamao.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Muwalimu amesema hayo Aprili 28, 2024 baada ya mbio za 'Run4Autism' (watoto wenye Usonji) za KM 5 zilizoanzia katika viwanja vya farasi kupitia daraja la Tanzanite Jijini Dar Es Salaam zikiongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa.

"Tumeanzisha na shahada ya kwanza ya Sayansi ya Saikolojia ya Kitabibu (Clinical Psychology) kuanzia mwaka huu wa 2024 lengo likiwa ni kuhakikisha huduma za utengemao zinapewa kipaumbele cha juu na Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan". Amesema Waziri Ummy
Waziri Ummy amesema, Serikali inaendelea kufanya juhudi za kutatua changamoto za watu wenye Usonji ambapo amebainisha miongoni mwa changamoto hizo hi pamoja na upungufu wa wataalam wa mazoezi tiba pamoja na gharama za mazoezi tiba kwa watu wenye Usonji.

"Tunategemea pia kuanzisha fani hizi katika ngazi Diploma kwa Mwaka wa fedha 2024/25 kwa kuwa nchi ni kubwa ili tuweze kuwa na watalaam wengi zaidi wa masuala ya 'Speech pathology', 'Occupational therapy', 'Physiotherapy' katika ngazi za vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya kote nchini.
Kwa upande wake Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Lukiza Autism Tanzania Bi. Hilda Nkabe ameishukuru Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Shahada hizo.

"Tunashukuru sana Serikali kwa kutuunga Mkono kwenye Taasisi yetu pamoja na kutambua watu wenye Usonji, tunaomba Serikali iendelee kuwapa kipaumbele hasa kwenye elimu pamoja na kazi za ufundi ambazo pia zinaweza kufanywa na watu wenye Usonji." Amesema Bi. Nkabe.

# Madaktari Sekoutoure wafanikisha kutoa jiwe la gram 800 kwenye kibofu cha mkojo

**Na Atley Kuni**
**MWANZA**

Madaktari wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza Sekoutoure wamefanikiwa kufanya upasuaji na kuondoa Jiwe ndani ya kibofu cha Mkojo kwa Mwanamke mwenye umri wa miaka 48.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa hospitalini hapo jiwe hilo lenye uzito wa Gramu 800 lilimsumbua mhusuka kwa zaidi ya miaka mitatu.

Akizungumza Aprili 18, 2024 na Daktari Bingwa wa Upasuaji katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza Sekoutoure Dkt. Jackson Chiwaligo amesema hiyo ni mara ya kwanza kufanya upasuaji kama huo.

Dkt. Chiwaligo ameeleza kuwa mgonjwa huyo alifika Hospitali ya Sekoutoure akiwa na changamoto ya kupata maumivu makali sehemu ya chini ya tumbo kwa zaidi ya miaka mitatu.

“Baada ya vipimo aligundulika kuwa na uvimbe mkubwa sehemu ya kibofu cha mkojo ulisababisha kufanyiwa upasuaji na kuondoa lenye uzito wa Gramu 800”, amebainisha Dkt. Chiwaligo

Dkt. Chiwaligo ambaye aliwaongza madakatafi wenzake amesema uwepo wa jiwe kwenye kibofu ni mkusanyiko wa madini ya chumvi ambayo hukauka na kusababisha uvimbe kutokea katika kibofu cha mkojo.
Kuhusu dalili za awali za tatizo hilo Dkt. Chiwaligo amesema dalili mbalimbali zinazosababisha ugonjwa huo kuwa ni pamoja na kukojoa mkojo uliochanganyikana na damu, maumivu makali chini ya tumbo na kushindwa kuzuia mkojo.

“Namna ya kujikinga na ugonjwa huu ni kwenda haja ndogo kwa wakati pale unapoipata na kunywa maji ya kutosha kwa wakati ” , ameeleza Dkt. Chiwaligo

Dkt. Chiwaligo ametoa wito kwa jamii kuwa na utaratibu wa kufika hospitalini kupata huduma za vipimo na kuwa na mtindo bora wa maisha ili kuepuka changamoto ya magonjwa kama hayo.





# Wananchi jiridhisheni na uhalali wa vituo vya huduma za Macho na Miwani Tiba

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DAR ES SALAAM**

Serikali imewataka wanachi kuchukua tahadhari ya huduma za Macho na Miwani tiba zinazotolewa ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kumkumba mtu ikiwepo kupoteza uoni au hata upofu.

Rai hiyo imetolewa na Baraza la Optometria Nchini Kupitia kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Dkt. Mohamed Mang'una, Aprili 19,2024 jijini Dar es Salaam.

"Nitumie fursa hii kwa wakazi wa Dar es Salaam na nchi nzima kwa ujumla kuhakikisha wanajiridhisha uhalali wa vituo na watoa huduma za tiba ya macho na miwani tiba kabla ya kupokea huduma yoyote ili kuepuka Madhara ikiwemo vifo na upofu wa kudumu" amesema Mang'una na kuongeza

"Jamii ijenge hulka ya kupitia mifumo rasmi ya utambuzi wa watoa huduma za optometria kupitia tovuti ya Mfumo wa Usajili wa Vituo vya afya wa Wizara ya Afya - HFRS ( hfrs.moh.go.tz)" amesisitiza Mang'una.

Amewataka wananchi, wasi sidanganyike, iwapo wana tatizo la macho, nenda kwenye vituo halali viliyosajiliwa kwa ajili ya huduma za Macho na Kioptometria (Miwani tiba).

Dkt. Mang'una ameongeza kuwa kwa Mkoa wa Dar Es Salaam huduma ya kupimwa au kupata miwani tiba inazidi kuimarika kwani jumla ya Vituo 89 vya optometria vimesajiliwa na pia hospitali zote za Serikali na binafsi zinatoa huduma hizi.

Kwa upande wake Msajili wa Baraza la Optometria Nchini, Sebastiano Millanzi amekemea kitendo cha watu wasio wanataaluma wa optometria kuvamia fani hiyo na kusisitiza Wataendelea ukaguzi wa kushtukiza mara kwa mara ili kuiepusha jamii na Waoptometria Vishoka.

"Vituo tulivyovifungia pia vimetozwa faini baada ya kukutwa na watoa huduma wasiokuwa na taaluma na wamili walio kinyume na sheria.

Nae Mwanasheria kutoka Wizara ya Afya, Abeli Mshashi amewakumbusha wamiliki na wale wote wenye nia ya kumiliki vituo vya kutolea huduma za Optometria kuhakikisha wafuata taratibu na sheria kwa mujibu wa sheria ya Optometria ya mwaka 2007.



# Zaidi ya wasichana milioni nne wenye miaka 9-14 kufikiwa na chanjo ya HPV

**Na Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imepanga hadi kufikia Disemba 2024 iwe imewafikia wasichana Milioni 4,841,298 wenye umri wa Miaka 9-14 kwa kuwapa dozi moja ya chanjo ya HPV baada ya kujiridhisha kuwa chanjo hiyo haina madhara na dozi moja inatosha.

Waziri Ummy amesema hayo Aprili 22, 2024 kwenye uzinduzi wa Maadhimisho ya Dozi moja ya chanjo ya HPV kwa wasichana wenye umri wa miaka 9 hadi 14 iliyozinguliwa katika viwanja vya Furahisha Wilayani Ilemela Mkoa wa Mwanza.

“Tutapita nyumba kwa nyumba, kitongoji, mtaa kwa mtaa, mjini, vijijini, kata kwa kata kwa kufikia lengo hili ili wasichana hawa waweze kupata chanjo ya HPV kwa lengo la kuwalinda na Saratani ya Mlango wa Kizazi”. Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummu amewapongeza Wakuu wa Mikoa kwa kupokea jambo hilo vizuri ambapo kwa kila Mkuu wa Mkoa amekuja na takwimu zake za kufikia idadi ya wasichana ambao watakuwa wamepata chanjo hiyo ya HPV.

“Tunakwenda kuijenga Tanzania isiyo na wagonjwa wa Saratani ya Mlango wa Kizazi, kuanzia Mikoa 10, 15, 30 inayokuja, hii ndio Tanzania ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa na Watanzania wenye Afya bora ili waweze kushiriki kwenye ujenzi wa familia zao na Jamii yetu kwa ujumla”. Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy ametoa wito kwa wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao kupata chanjo hiyo maana kuwaficha ni kumnyima haki yake ya msingi ya kuwa na Afya bora.

“Lengo letu tunataka kufikia 90% inapofika Mwaka 2030 kwa Binti yoyote anapofikia umri wa miaka 14 awe amepata chanjo ya HPV na kuhakikisha tunafanya uchunguzi wa mapema dhidi ya Saratani ya Mlango wa Kizazi kwa kufikia 70%”. Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy ametoa wito kwa wanawake wote hususan wenye umri miaka 25-49 kufanya uchunguzi wa Saratani ya Mlango wa Kizazi angalau mara moja kwa mwaka kwa kuwa ugonjwa huo unapona iwapo utagundulika mapema.

“Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuwezesha, tumepeleka vifaa vya kupima na kutibu mabadiliko ya awali ya Saratani ya Mlango wa Kizazi mpaka ngazi ya Zahanati, hii ni hatua kubwa kwa Tanzania”. Amesema Waziri Ummy




# Hospitali Mount Meru yatakiwa kuimarisha ulezi Vituo vya Afya

**Na Shaban Juma**
**ARUSHA**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, ametoa wito kwa uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha, Mount Meru, kuimarisha ulezi wa vituo vyote vinavyotoa huduma za afya ikihusisha huduma za mkoba na mafunzo kwenye utoaji wa huduma za afya ili kuimarisha na kuboresha huduma za afya.

Dkt. Jingu ameyasema hayo , Aprili 15, 2024 Mkoani Arusha wakati wa ziara yake katika Hospitali hiyo kwa lengo la kuangalia hali ya utoaji huduma.

“Tuimarishe ulezi wa vituo vingine vyote vinavyotoa huduma za afya hapa mkoani na ulezi huku mkihusisha huduma za mkoba na mafunzo katika vituo vya kutolea huduma za afya". Amesema Dkt Jingu

Pia, Dkt. Jingu Amesema ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi, Mount Meru inatakiwa kuwa Hospitali kiongozi katika mkoa huu kwa kuwajengea uwezo watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Dkt. Jingu ameongeza kuwa kulea vituo vingine chini ya uongozi wa Hospitali ya

Mount Meru kutahakikisha mkoa mzima unanufaika na viwango vya juu vya huduma za afya.

"Ulezi huu hautahusisha tu upatikanaji wa vifaa tiba na rasilimali watu bali pia mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyakazi wa afya ili kuendeleza stadi zao na kuboresha huduma wanazotoa" amesisitiza Dkt. Jingu.
Awali akisoma taarifa ya Hospitali Kaimu mganga mfawidhi wa Hospitali ya Mount Meru Dkt. Kipapi Mlambo amemshukuru Dkt. Jingu kwa kutembelea hospital hiyo na kukagua hali ya utoaji wa huduma kwani kufanya hivyo ni chachu ya watumishi katika sekta ya afya kufanya kazi kwa weledi zaid.

# Tuepuke tabia bwete kukabiliana na magonjwa Yasiyoambukiza.

**Na Atley Kuni**
**ARUSHA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imewaasa watumishi wa umma, binafsi na jamii kwa ujumla kuhakikisha wanaepukana na tabia bwete ili kukabilina na Magonjwa yasiyoambukiza.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu ametoa rai hiyo wakati kikao cha Makatibu Wakuu kilicholenga kujadili afua jumuishi za kuzuia na kudhibiti Magonjwa yasiyoambukiza April 5, 2024 ambapo amezisihi Wizara za kisekta na wadau kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuja na ajenda ya kitaifa juu ya kudhibiti Magonjwa yasiyoambukiza.

"Tuhamasishane kuanzia maofisini kuacha tabia bwete na tuwe na hulka ya kufanya mazoezi, tuwe na siku maalum ya matembezi kwenda kazini, Mfano, Wizara ya Afya kwa wiki itenge siku tatu za kufanya mazoezi jioni. Hii itatufanya kuwa na Afya bora". Amesema Dkt. John Jingu.

Dkt. Jingu ameongeza kuwa wizara na sekta ya afya kufikiri mbali zaidi na kuunda mikakati madhubuti ya kuhamasisha watanzania kubadili mitindo wa maisha.

Akizunguza kwenye kikao hicho Daktari bingwa na katibu wa chama cha magonjwa yasiyoambukiza Prof. Kaushik Ramaiya amesema lazima jamii ijue magonjwa yasiyoambukiza yanaweza kuzuilika kwa kutoa elimu kwa jamii ili wabadilishe mitindo ya maisha yao kwa kuzingatia mazoezi na ulaji wa vyakula vyenye lishe bora.

Awali akitoa wasilisho Mtaalam wa Sheria za Afya Bw. Augustus Fungo amesema ili kuweza kudhibiti ulaji vyakula vyenye sukari, chumvi na mafuta, Serikali itaendele kutilia mkazo uwekwaji wa taarifa sahihi katika vifungashio vya vyakula, kumpa machaguo mwananchi huku akitilia mkazi kwa serikali kuunda sheria kuongeza kodi kwenye vinywaji vyenye sukari, chumvi nyingi ili kupunguza matumizi ya vitu hivyo.

"Vyakula tunavyonunua kwenye maduka ya bidhaa za vyakula hawaweki taarifa za vitu vilivyotumika kwenye kutengeza vyakula hivyo , hivyo serikali ikitilia mkazo kwenye hili litampa machaguo mwananchi pale anapoona kuwa chakula kina mafuta, sukari au chumvi nyingi, pia kuongeza pei ya kodi ya vinywaji wenye sukari hii itafanya vinywaji hivyo kiuzwa kwa bei ya juu sokoni na kumfanya mwananchi kutotumia vinywaji hivyo". Amesema Bw. Fungo.



# Dozi moja ya chanjo ya HPV inatosha kumkinga Msichana kupata Saratani ya Mlango wa Kizazi



**Na Aisha Swahibu**
**MWANZA**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema dozi Moja ya chanjo ya HPV inatosha kumkinga msichana kupata ugonjwa wa Saratani ya Mlango wa Kizazi na kuwataka wazazi/walezi kuwapeleka watoto kupata chanjo hiyo.

Waziri Ummy Mwalimu amesema hayo Aprili 22, 2024 kwenye uzinduzi wa Maadhimisho ya Dozi moja ya chanjo ya HPV kwa wasichana wenye umri wa miaka 9 hadi 14 iliyozinguliwa katika viwanja vya Furahisha Wilayani Ilemela Mkoa wa Mwanza.

“Wataalamu wetu ambao wanatoka kwenye Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) wametuhakikishia kuwa dozi moja ya chanjo ya HPV inatosha kumkinga msichana kupata Saratani ya Mlango wa Kizazi”. Amesema Waziri Ummy

Amesema, awali dozi zilizokuwa zinatolewa mbili, ya kwanza inatolewa na baada ya miezi Sita inatolewa nyingine hii ilikua inapelekea mabinti wengi kutorudi kupata dozi ya pili, Sasa hivi tumeamua kutoa dozi moja ya HPV kwa kuwa inatosha kuwakinga wasichana kuja kupata maambukizi ya Saratani ya Mlango wa Kizazi.

Aidha, Waziri Ummy amesema Saratani inayoongoza kuwatesa Watanzania ni Saratani ya Mlango wa Kizazi ambapo amesema katika kila wagonjwa 100 wanaougua Saratani, wagonjwa 23 ni wagonjwa wa Saratani ya Mlango wa Kizazi.

“Inafuata Saratani ya mfumo wa chakula asilimia 11, Saratani ya Matiti asilimia 10.4, Saratani ya tezi dume asilimia 8.9 kwa hiyo ukiaangalia hapo Saratani inayoongoza ni Saratani ya Mlango wa Kizazi”. Amesema Waziri Ummy
Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Mhe. Amina Makilagi akimuwakilisha Mkuu wa Mkoa Mwanza Mhe. Saidi Mtanda amesema watahakikisha watoto wote wenye umri wa kuanzia miaka 9-14 wanapata chanjo hiyo ili kufikia malengo.

“Kwa mwaka 2022/23 Mkoa wa Mwanza ulifanikiwa kuchanja watoto zaidi ya laki Mbili sawa na asilimia 107 kati ya walengwa waliotarajiwa kuchanjwa ni laki 191,440 wenye umri chini ya Mwaka Mmoja, tumefikia malengo na kuyavuka”. Amesema Mhe. Makilagi

# Tehama iwe kichocheo kwenye tathmini na ufuatiliaji wa takwimu - Dkt. Jingu

**Na Atley Kuni**
**ARUSHA**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amesema Matumizi na Teknojia ya habari iwe ni kichocheo cha kufanya ufuatiliaji na tathmini ili kupata takwimu sahihi zitakazo changia kufanya maamuzi sahihi wakati wa kuandaa mipango ya bajeti kwenye Sekta ya Afya.

Dkt. Jingu amesema hayo wakati akifungua kikao cha siku mbili, Aprili 15, 2024 jiji Arusha, kilichowakutanisha wataalam wa Tehama na wale wa ufuatiliaji na tathmini zaidi ya 70 kwa lengo la kukuza ushirikiano baina ya wadau hao, uboreshaji wa program na maende ya jumla ya utoaji wa huduma kwenye kwenye sekta ya afya ili kuwa na takwimu sahihi.

Dkt. Jingu amesema ukuaji wa Teknolojia uende sambamba na mabadiliko ya mifumo ya TEHAMA kwa kuiunganisha ili iweze kusomana hali itakayochangia kuwa na tija na ufanisi wakati wa utekelezaji wa majukumu kwenye sekta afya na kupata matokeo chanya.

"Chochote tunachofanya katika dunia ya lazima tutumie TEHAMA, kwetu sekta ya afya hii ni ajenda muhimu sana kutokana na unyeti wa shughuli zetu, kosa moja linaweza kusababisha kukosekana kwa huduma, ulemavu na wakati mwingine kupoteza uhai wa mtu, hivyo kikao kazi hiki kitumike kutoka na maazimio yatakayokuwa na tija na ufanisi". Amesema Dkt. Jingu.

Dkt. Jingu amesisitiza juu ya mifumo ya Tehama kutengenezwa kulingana na mahitaji na kuzingatia teknolojia mpya na ya kisasa. "Tusikimbilie kuanzisha mifumo mingi, tutumie mifumo iliyopo tuiboreshe ili iendane na wakati, mtakumbuka Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, hivi karibuni alihimiza matumizi ya TEHAMA, sasa mnapokuwa na kikao hiki cha siku mbili mhakikishe mnachukua kama sehemu ya fursa ya majadiliano yenu muweze kutoka na maazimio." Amesema Dkt. Jingu.

Akizungumza wakati wa kikao hicho Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) hapa nchini Dkt. Charles Moses amesema dunia imekuwa na mabadiliko mengi kwa muda mfupi, hivyo kila mabadiliko yanapotokea hususan ni kwenye Teknolojia ya habari na mawasiliano lazima vilevile na utendaji uendane na mabadiliko hayo.






MAKALA MAALUM

# Mapambano ya Kifua Kikuu iwe vita ya wote

**Na Atley Kuni**

Tanzania ambayo inatajwa kuwa miongoni mwa nchi 30 zinazochangia asilimia 87 ya wagonjwa wa kifua kikuu duniani, imejiwekea lengo la kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu kwa asilimia 75 na kupunguza visa vya Kifua Kikuu kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2025.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2023 zinaonesha kuwa kuwapo kwa wagonjwa wapya wa kifua kikuu wapatao milioni 10.6 duniani na kati ya hao wagonjwa milioni 1.3 sawa na asilimia 13 walifariki.

Wakati takwimu za dunia zikionesha hivyo, Tanzania kulikua na wagonjwa wapya wa kifua kikuu 128,000 sawa na wagonjwa 195 kwa kila watu 100,000 ikionesha maambukizi kupungua kwa asilimia 36 ikilinganisha na miaka saba iliyopita na vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu vilikuwa 18,100 vikiwa vimepungua kwa asilimia 69 ikilinganishwa na mwaka 2015.

Kupungua kwa maambukizi mapya na vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu hakuwezi kuifanya nchi ikaweka miguu chini bila kuendelea kuchukua hatua madhubuti kwa kuwekeza katika afua stahiki ili kufikia

malengo tuliojiwekea la kuutokomeza kabisa ugonjwa huo ifikapo 2030.

Akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani inayoadhimishwa kila Machi 24 Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alinukuliwa. akisema Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau na sekta ya afya wamejipanga kuchukua hatua za makusudi za kuweza kuwafikia na kuwaweka kwenye matibabu ya kifua kikuu kwa asilimia 90 ya wagonjwa wote wanaokadiriwa kuwepo ifikapo mwaka 2025.

“Kufikia hii asilimia 90 sio jitihada za Wizara pekee zinazohitaji bali jitihada za pamoja na zenye msukumo wa dhati kuona Kifua Kikuu kinakuwa historia kwenye Taifa la Tanzania. Na

ataona wajibu wa kujitolea kwa hali na mali ili kuweza kuwafikia na kuwaibua wagonjwa wengi na kuwaweka katika matibabu ili kufikia malengo yetu ya kutokomeza ugonjwa huu". Amesema.

Waziri Ummy ameongeza kuwa mgonjwa mmoja wa kifua kikuu ambaye hajagundulika na kuwekwa katika matibabu ana uwezo wa kuambukiza watu kati ya 10 mpaka 20 kwa mwaka.

Piga picha ya mgonjwa mmoja mwenye vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu yupo miongoni mwa wasafiri wa mwendokasi iliyosheheni abiria au kwenye mikusanyiko na mikutano ya watu wengi kama sokoni, mialoni, kwenye kumbi za starehe kwa kutaja baadhi.

Wengi tunajua mazingira ya kwenye machimbo, mahabusu zetu, viwanja vya mipira, safari za watalii, kumbi za kuangalia sinema, makambi ya wakimbizi, mikusanyiko ya kisiasa, mabweni ya wanafunzi, makambi ya wavuvi, wazee na watoto yatima pamoja na makazi holela.

Nimejaribu kuanisha sekta tofauti tofauti, ili uweze kupata picha kuwa, tunapozungumza vita hii ni ya watu wote tuone ukubwa wa tatizo, fikiria kauli ya Waziri Ummy, halafu piga picha mtu mmoja aliyepo kwenye kanisa moja la maombezi tuone ukubwa wa tatizo.

Tuwaze juu ya biashara kubwa ya utalii ambayo inaliingizia fedha za kigeni taifa, labda uwepo wa muongoza watalii mmoja aliye na vimelea vya kifua kikuu, huku akiwa na kikundi cha watu 10 ina maana anaweza kuwaambukiza wote.

Pia tuangalie kwa jicho la tatu, sehemu za uchimbaji wa madini mbalimbali ambazo zina mikusanyiko ya watu, sio hiyo tu fikiria msanii wa muziki aliyeandaa tamasha lililo waleta watu zaidi ya 1000 kwa wakati mmoja. Pata pia picha ya abiria waliokatika madaladala na mwendokasi uliosheheni wakasafiri kila siku katika shughuli zao za kila siku.

Hapa ndipo ninapokuja na wazo kuwa vita ya kifua kikuu sio ya mtu au kundi fulani bali wadau wote kwa nguvu moja kutafuta rasilimali, kubuni afua mpya, kutoa elimu kwa kila sekta,
Mbali na miongozo iliyopo na mikakati yakukabiliana na Kifua Kikuu kwa sasa, kila nyenzo inayo onekana kufanikisha mapambano, itumike kwa maslahi mapana ya nchi.

Serikali kupitia Wizara ya Afya imefanya juhudi za kudhibiti ugonjwa huu kwa kuboresha huduma za uchunguzi na uugunduzi kufuatia kuwekeza katika tekinolojia mpya pamoja lakini pia kusambaza magari 11, mashine za Gene Xpert 50, Mashine za ECG 179 na pikipiki 179 zenye thamani ya Sh bilioni 6.8. hivi vyote ni rasilimali vitu.

Pia wajumbe wa kikao cha waratibu wa dawati linaloshughulikia kifua kikuu kwenye Wizara za kisekta waliokutana kwa siku mbili jijini Dodoma wanakuja na maazimio ambayo yanazidi yakuonesha mwanga wa kuzidi kupambana na kifua kikuu.

Baadhi ya kile kilichoadhimiwa katika mapambano ya dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu kuwa ni kuwa na elimu endelevu kwenye maeneo ya kazi, kuwa na taarifa za mara kwa mara zinazo elezea afua zilizo tekelezwa katika Wizara au Sekta husika.

Pia uhuishaji wa lengo la kila Wizara kuanisha wadau ambao itashirikiana nao bega kwa bega katika vita ya kutokomeza kifua kikuu nchini ni hatua muhimu sana na za kuigwa mfano.

Baada ya kuangalia ukubwa wa tatizo ni busara kila sekta kuunga mkono juhudi za Wizara ya Afya za kupambana na ugonjwa wa kifua kikuu kwa kuwekeza katika kutekeleza afua za kisekta zinazojielekeza katika vita hii.

Kupanga nikuchagua, iwapo sekta zote zitasimama kidete kuhakikisha wanakuwa mabalozi wa kukabiliana na ugonjwa huu, vita hii itafanikiwa na malengo yaliyowekwa yatatimia. Kifua kikuu kina kinazuilika na kinatibika, sote tuwajibike.





# Madaktari bingwa wa Rais Samia wafanya makubwa Geita, Tanga, Morogoro na Ruvuma.

**Na Shaban Juma**

Madaktari Bingwa na Bobezi wa Rais Samia wanao kwenda na kauli mbiu imesemayo "Tumekufikia Karibu Tukuhudumie" wameanza kwa kufanya mambo makubwa kwa Mikoa ya Geita, Tanga, Ruvuma na Morogoro kwa kubadilishana uzoefu, ujuzi ambao umeongeza tija na ufanisi katika utendaji wa kazi kwa madaktari wegine.

Wakizungumza kwa Nyakati tofauti wamesema, kambi ya Madaktari Bingwa iliyoanza Aprili 29, 2024 imewawezesha madaktari kubadilishana uzoefu pamoja na kutatua changamoto za wagonjwa kwa wakati.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mifupa Mkoani Geita Dkt. Zablon Saguta amesema ndani ya siku Moja (Aprili 30, 2024) wamekutana na wananchi wenye shida ya mifupa wapatao 70 ambapo Idadi hiyo itaweza kuongezeka kutokana na wananchi kuendelea kupata taarifa ya ujio wa madaktari hao.

Akifungua kambi hiyo mkoani Tanga, Mkuu wa Mkoa wa huo Balozi Dkt. Batilda Buriani amesema madaktari Bingwa na Bobezi wa Rais Dkt. Samia zaidi ya 30 wamefika Mkoani humo kusaidiana na madaktari 60 waliopo ambapo watu zaidi ya 700 wamejitokeza na kupatiwa huduma za matibabu.

Taarifa kutoka Nyanda za Juu Kusini iliyokita kambi Mkoani Ruvuma inasema zaidi ya wananchi 3,500 wenye changamoto za magonjwa mbalimbali wa Mkoa huo na maeneo ya jirani nao wamejitokeza kwenye huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima wakati akiongea na waandishi wa habari kuelekea zoezi hilo katika Mkoa huo amesema Madaktari Bingwa na Bobezi 56 wanatarajia kushiriki kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa wananchi zaidi ya 2000 wa Mikoa ya Morogoro, Iringa, Singida, Dodoma na Pwani kupitia kambi maalum ya matibabu ya siku Tano ndani ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro kuanza tarehe 6 Hadi 10 Mei, 2024.

Miongoni mwa magonjwa yatakayotolewa huduma katika kambi za madaktari Bingwa na Bobezi ni pamoja na magonjwa ya akina mama na uzazi, magonjwa ya ndani kama vile shinikizo la damu, Kisukari, Figo, magonjwa ya watoto, mifupa, upasuaji, macho, kinywa na meno, pua na koo, upasuaji wa watoto wenye midomo sungura, masikio, ngozi, moyo, mfumo wa chakula pamoja na magonjwa ya Saratani.

# Kambi ya madaktari bingwa, bingwa bobezi imestawisha utendaji wa kazi Geita

**Na Atley Kuni**
**GEITA**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya ndani wa Hospitali ya Rufaa Geita Dkt. Sabrina Kumlin amesema Kambi ya Madaktari Bingwa na Bingwa Bobezi imestawisha utendaji wa kazi kwa kuongeza tija na ufanisi katika utendaji wao.

Dkt. Sablina pamoja na wataalamu wengine wakizungumza kwa Nyakati tofauti wamesema, Kambi ya Madaktari Bingwa iliyoanza Aprili 29, 2024 imewawezesha madaktari kubadilishana uzoefu pamoja na kutatua changamoto za wagonjwa kwa wakati.

"Jopo hili la Madaktari, uzofu wetu unatofautiana, yawezekana mimi nikakutana na jambo kwa mara ya kwanza, lakini tatizo hilo hilo mwenzangu alisha kutana nalo kabla, hivyo tunashauriana kwa haraka na kupata ufumbuzi." Amesema Dkt. Sabrina

Kwa upande wake Daktari Mbobezi wa wanawake na uzazi Dkt. Ndulila Samweli wa Hoapitali ya Sekouture Mwanza, amesema, hatua yakuwafikia wananchi kwenye maeneo yao imewawezesha wengi kujitokeza.

"Huduma hizi za mkoba tungezishusha hadi ngazi ya Wilaya kwa kuwa uzoefu unaonesha wanachi wengi hushindwa kutoka kwenda mbali kupata matibabu na kumfanya mgonjwa kuendelea kujenga usugu wa ugonjwa, lakini tunapowafuata wengi wanajitokeza." Amesema Dkt. Ndulila.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mifupa Dkt. Zablon Saguta amesema ndani ya siku Moja wamekutana na wananchi wenye shida ya mifupa wapatao 70 kwa haraka, sio rahisi watu wote hawa kuhudumiwa na mtu mmoja.

"Idadi hii itaweza kuongezeka kutokana na wanachi kupeana taarifa hivyo unaweza kujiuliza watu wote hao walikuwa na matatizo ya mifupa lakini wameibuliwa na kambi hii ya huduma ya Mkoba." Amesema Dkt. Saguta

Katika hatua nyingine, Mwalimu mstaafu Bibi Ester Kizuguto ambae ni mkaazi wa Kata ya Mkolani Wilaya ya Geita na mkoani Geita, ameishuru Serikali kwa hatua yake yakusogeza huduma za mkoba za Madaktari Bingwa na Bobezi kwani zimewarahisishia huduma.

Jumla ya Madaktari Bingwa, Bingwa Bobezi 32 wapo Mkoani hapo kuanzja Aprili 29 hadi Mei 3, 2024 kwa ajili ya kuhudumia wananchi kwa kaulimbiu isemeyo "Madaktari wa Dkt. Samia Kanda ya Ziwa Tumekufikia, Karibu Tukuhudumie."



# Fahamu Namba Zako

Pima uwiano wa urefu na uzito wako

Pima Presha

Pima Sukari

*"Afya Yangu, Haki Yangu"*

***#UsijisahauJaliAfyaYako #BadiliMtindoWaMaisha***

Kwa Taarifa, Elimu na Ushauri zaidi, Piga simu namba 199 Bure




**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI APRILI, 2024**